**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI GEITA**

Mtaa wa Bomani, S.L.P 477, Geita. TANZANIA. Simu: 0282520296,
Nukushi 0282520159, Barua Pepe: info@geuwasa.go.tz, md@geuwasa.go.tz
Tovuti: www.geuwasa.go.tz


# TAARIFA YA HALI YA HUDUMA YA MAJI

# APRILI, 2024

## 1. UTANGULIZI

- Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Geita (GEUWASA) iliundwa chini ya sheria ya maji “The Waterworks Act Cap. 272” ambayo ilifanyiwa marekebisho (mwaka 1997 G. N. No. 371) na sheria mpya ya Maji Na. 12 ya Mwaka 2009 “The Water Supply and Sanitation Act, 2009 na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali Na. 258 la tarehe 02 Juni 2002. Chini ya sheria hii, Mamlaka imepewa majukumu ya kutoa huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Geita.
- Tuna kanda 6 kwa sasa ambazo ni Kasamwa – Kanyala, Chigunga, Nyankumbu,Mwatulole,Mjini Kati na Nyankumbu.

- Mji wa Geita una wakazi wasiopungua **361,671** na idadi ya wakazi wanaopata huduma ya maji kutoka Mamlaka ya Maji ni asilimia **75%** tu sawa na wakazi **237,503** ambao wapo katika maeneo yaliyopitiwa na mtandao wa maji.

- Maeneo ambayo hayajafikiwa na mtandao yanapata huduma ya maji kupitia visima vilivyofungwa pampu ya mkono na visima vya asili.
- Vyanzo vya maji – Visima virefu , Chemichemi,Ziwa Viktoria na Bwala maji la Nyankanga.

- Pia taasisi yetu inaongozwa kwa kuzingatia miongozo mbalimbali na inasimamiwa na ofisi ya TRO na EWURA

# 3. MIUNDOMBINU YA MAMLAKA

- **Matenki ya Maji**

Mamlaka ina jumla ya matenki 19 ambayo yana uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 3,345 ambayo yamejengwa katika maeneo tofauti tofauti.

- **Mitandao ya Maji**

Mamlaka ina mtandao wa mabomba ya maji wenye urefu wa kilometa 396.57 yenye kipenyo cha 350mm – 50mm.


- **Vituo vya kuchotea Maji**

Mamlaka ina jumla ya vituo vya kuchotea maji 122 ambavyo vimeunganishwa na huduma ya maji.


# HALI YA WATUMISHI

| Na. | Aina ya Ajira | Idadi ya Watumishi Waliopo | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Ke | Me | Jumla |
| 1. | Ajira ya Kudumu | 15 | 22 | 37 |
| 2. | Ajira za Muda Maalum | 8 | 35 | 43 |
| | **Jumla** | **23** | **57** | **80** |

# IDADI YA WATEJA


Wateja
12
10
8
6
4
2
0
5
7
8
10
11
2018/2019
2019/2020
2020/2021
2021/2022
2022/2023

# MAKUSANYO


MAKUSANYO (Milioni)
KIASI (MIL)
3
3
2
2
1
1
500
0
857
609
1
919
2
1
2
1
2
1
3
2
2017/2018
2018/2019
2019/2020
2020/2021
2021/2022
2022/2023
MWAKA WA FEDHA
Malengo
Kiasi cha makusanyo

# 4. USIMAMIZI NA UJENZI WA MIRADI MBALIMBA KATIKAMWAKA WA FEDHA 2023/2024

## 4.1. **UJENZI WA MRADI WA MAJI  BUNG’WANGOKO**

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka ilianza ujenzi wa Mradi wa kusambaza maji Bungw’angoko ambao ukikamilika utanufaisha wakazi wapatao 6,200 wa maeneo ya Mshinde, Chabulongo na  Bungw’angoko. Mradi huo unagharimu jumla ya TZS Mil 569 na utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 35.



## 4.2. UJENZI WA MRADI WA MAJI BULELA - NYASEKE

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka imeanza ujenzi wa Mradi wa kusambaza maji Bulela-Nyaseke ambao ukikamilika utanufaisha wakazi wapatao 5,000 wa maeneo ya Bulela-Nyaseke. Mradi huo unagharimu jumla ya TZS Mil 445. kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo;

i. Ujenzi wa tenki la maji lenye ujazo wa lita 135,000
ii. Ujenzi wa mtandao wa kusambaza maji kilometa 4
iii. Ujenzi wa mtandao wa kusafirisha maji kilometa 9
iv. Ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 6
v. Ujenzi wa nyumba ya pampu
vi. Ujenzi wa mkondo wa umeme na ununuzi wa transfoma 50 kVA



## 4.3. UTANUZI WA MTAMBO WA KUTIBU MAJI NYANKANGA

- Mamlaka imeendela na ujenzi wa utanuzi wa mtambo wa kutibu maji eneo la Nyankanga wenye thamani ya **TZS Bilioni 1.1**
- Utekelezaji wa Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili kama ifuatavyo;
  i. Ununuzi wa pampu yenye uwezo wa kuzalisha lita 300,000 kwa saa – **TZS Milioni 199**
  ii. Upanuzi wa miundombinu ya kutibu maji - **TZS Milioni 812**

- Hadi sasa utekelezaji wa kazi zote umefikia **asilimia 95** na jumla ya kiasi cha **TZS Milioni 988,863,866.08** ambapo (Kiasi cha **TZS Milioni 789,287,595.00** zimelipwa kwa Mandarasi wa kazi za ujenzi wa utanuzi wa Chujio na kiasi cha **TZS cha Milioni 199,576,271.19** malipo ya mzabuni wa pampu).

# UTEKELEZAJI WA MRADI WA NYANKANGA KATIKA PICHA





## 4.4. UJENZI WA MRADI WA KUBORESHA HUDUMA YA MAJI KATIKA MJI WA KATORO-BUSERESERE

- Mradi huu umelenga kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji katika kata za Katoro, Buserese, Nyamigota na Ludete. Mradi huu unatekelezwa kwa *Force Account* kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita kwa gharama ya **TZS Bilioni 6,617,314,331.00**
- Mpaka sasa utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 95** na jumla ya kiasi cha **TZS 6,382,314,331** zimelipwa na mradi upo katika hatua ya majaribio.







Champion

## 4.5. UJENZI WA MRADI WA MAJI KUTOKA ZIWA VICTORIA

- Serikali ilianza utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Miji 28 kwa Miji ya Geita na Chato Mkoani Geita. Kwa upande wa Geita mjini, Mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Aprili, 2023 na muda wa utekelezaji ni Miezi 32. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2025.
- Mkandarasi ***M/s Afcons Infrastructure Limited JV Vijeta Projects and Infrastructures Limited*** *pamoja na Mtaalamu Mshauri* ***WAPCOS LIMITED wanatekeleza mradi huu*** kwa gharama ya Dola za Marekani **Milioni 53.463 kwa Mji wa Geita**. Kazi zinazotekelezwa ni;
  - Ujenzi wa tenki la maji lita 5,000,000 eneo la Geita Hill na tenki la 2,000,000 eneo la mpomvu.
  - Ujenzi wa matenki matatu (3) yenye ujazo wa lita 1,900,000 Geita vijijini ambapo vijiji 19 vitanufaika.
  - Ujenzi wa mtambo wa kutibu maji wenye uwezo wa lita 44,000,000 kwa siku.
  - Ujenzi wa mtandao wa kusambaza maji km 30 eneo la Geita mjini.
  - Ujenzi wa mtandao wa kusafirisha maji km 56.

**Mpaka sasa utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 20.**


GEITA HILL STK
5,000,000 LTRS


KAGU ST
1,000,000 LTRS


SENGA ST
700,000 LTRS


MPOMVU ST
2,000,000 LTRS

## 6. CHANGAMOTO ZINAZOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI

- Fedha za miradi ya maji kutoka Wizarani kutolipwa kwa wakati na kusababisha miradi mingi kutokamilika kwa muda uliopagwa.
- Kusuasua kwa utekelezaji wa miradi kwa baadhi ya Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji.
- Kuchelewa kwa fidia baadi ya maeneo ya ujenzi yanayohitaji gharama za fidia.
- Kuchelewa kwa msamaha wa kodi kwa baadhi ya miradi.
- Gharama kubwa za dira za maji za wateja
- Gharama kubwa za uendeshaji ukilinganisha na bei za maji

***AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA***